

Shairi lifuatalo liliandikwa na Malenga Hamidu Tambwe miaka kadha iliyopita likizungumzia umuhimu wa utunzi mzuri wa mashairi na nasaha za kimaisha

HAMNA MAENDELEO HAYA YAKISHAMIRI

1. Mhisani Editori, Tambwe ninakuja mbio,
Niambe nno fikiri, ela pasina kemeo,
Niutoe ushauri, kuhusu mambo yajayo,
Hamna maendeleo, haya tukiyashamiri.
2. Haya tukiyashamiri, hapana maendeleo,
Bora kuwa penye hari, na baridi na mawio,
Kutunga kwa umahiri, kutatoa fanikio,
Hamna maendeleo, haya tukiyashamiri.
3. Haya tukiyashamiri, kwamba yapatikanayo,
Utaghibu uhodari, pasiwe mafanikio,
Muda sasa umejiri, uchape na mengineyo,
Hamna maendeleo, haya tukiyashamiri.
4. Kwetu sisi ni fahari, kukuza tuliyonayo,
Tuyatunge mashairi, ya namna nyingineyo,
Uyatote editori, katika kila toleo,
Hamna maendeleo, haya tukiyashamiri.
5. Tarbia zakithiri, katika zako toleo,
Mengine hayadhihiri, kati yapatikanayo,
Itafaa mhariri, ufanye mchanganuo,
Hamna maendeleo, haya tukiyashamiri.
6. Takhmisa nzuri nzuri, tathinina zije mbiyo,
Malenga walo mahiri, watoe utunzi wao,
Uchape kila dahari, tunzi za namna hiyo,
Hamna maendeleo, haya tukiyashamiri.
7. Jibu ninalisubiri, nijue uyapendayo,
Nijibu kwa ikrari, tena pasipo uchoyo,
Ili utunzi ujiiri, tupate mafanikio,
Hamna maendeleo, haya tukiyashamiri.

Hamidu R. Tambwe (1968)